

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo Na. 1

Jan - Machi 2021

## Waziri Mkuu: Waajiri toeni kipaumbele makato elimu ya juu

*Na Mwandishi Wetu*

**Waziri** Mkuu Kassim Majaliwa amewataka waajiri wa sekta binafsi na umma nchini kutoa kipaumbele kwa makato ya mikopo ya elimu ya juu kama yalivyo makato mengine ya kisheria.

Akitoa hoja ya kuhairisha Bunge jijini Dodoma tarehe 13 Februari mwaka huu, Waziri Mkuu alisema kwa kufanya hivyo, utaratibu wa urejeshaji mikopo utaongeza maradufu idadi ya wanufaika wa mikopo hiyo katika miaka ijayo.

Majaliwa alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali imefanya mageuzi makubwa ya mifumo ya utendaji katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na hivyo kusaidia kuongezeka kwa makusanyo ya mikopo kutoka TZS 28 Bilioni mwaka 2016/17 hadi TZS 192 Bilioni mwaka 2019/2020.

**Inaendelea UK7**



## 'Mtoto' Kazaliwa, Tumsome!



**Ismail Ngayonga**  
Mhariri

**Kwa** dunia ya leo, ni sahihi kabisa kusema kwa kutumia 'simu janja' ni chanzo muhimu cha mawasiliano na kupeana taarifa.

Ndiyo sababu, wewe msomaji wetu, umeweza kumpokea 'mtoto' huyu mpya aitwaye 'HESLB Yako' na sasa unamfurahia kwa kutumia 'simu janja' yako. Tunakusihhi umpokee, umsome na utupe maoni.

Ukweli ni kuwa matumizi ya mitandao ya kijamii ni mojawapo ya jukwaa kubwa la mawasiliano linalounganisha huduma na shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi duniani kwa sasa.

Inakadiriwa kuwa hadi kufikia mwaka 2018 pekee, watu zaidi ya bilioni 2.65 walikua watumiaji wa mitandao duniani, huku mashirika na taasisi za umma na binafsi zikitumia majukwaa hayo kwa ajili ya kufikia wateja wake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), hadi kufikia machi 2020, idadi ya watumiaji wa huduma

za mtandao nchini imeongezeka hadi kufikia milioni 26.8 na kundi kubwa likiwa ni vijana.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeanzisha jarida la mtandaoni la 'HESLB Yako' ambalo litachapishwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali wa elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini ambao idadi yao kubwa ni watumiaji wa mitandao ya kijamii.

'HESLB Yako' linatarajia kuwa jukwaa maalum litakalotumika kuharakisha mawasiliano baina ya HESLB na wadau kwa kutoa taarifa, kubadilishana uzoefu, kupokea maoni na ushauri kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji wa HESLB.

Tuandikie kwa barua pepe: [adcp@heslb.go.tz](mailto:adcp@heslb.go.tz) na usite kutembelea kurasa zetu za za mitandao ya kijamii kama zinavyoonekana hapa chini.

**Furahia!**

NDANI...



01



03



06



07



10





**Abdul-Razaq Badru**  
Mkurugenzi Mtendaji - HESLB

## Karibu & Furahia HESLB Yako!

**Dhamira** yetu ni kukushirikisha na kupokea maoni yako ili kuboresha huduma zetu.

Ni kwa kuzingatia hili, tumekuwa tukitekeleza Mpango Mkakati wetu wa miaka mitano (2017/2018 – 2021/2022) ambao unaongozwa na nguzo kuu tatu: Mosi, Kuboresha mifumo ya uendeshaji (Business Processes Re-engineering); Pili, Kukusanya na kutoa mikopo zaidi (Optimal Lending & Collection); na tatu Kuimarisha mahusiano ya kimkakati (Strategic Partnerships).

Ili kutimiza nguzo hizo, wewe msomaji ni mdau muhimu sana kwetu. Ninakusihia utumie muda wako kusoma na kutupatia maoni kupitia mawasiliano yaliyopo katika jarida hili. Tunakuahidi tutayafanyia kazi.

Jarida hili litakuwa likichapishwa mara nne kwa mwaka, kila baada ya miezi mitatu. Kwa kuwa hili ni jarida la kwanza mtandaoni, ninaomba nikushirikishe masuala kadhaa katika utekelezaji wa mpango mkakati wetu.

Mosi, uboreshaji mkubwa wa mifumo umeendelea kwa awamu mbili, (Grand Automation & Systems Intergration Phase I & II). Kwa sasa maombi ya mikopo yanafanyika kwa mtandao na mwombaji anapata taarifa kupitia akaunti yake mtandaoni. Katika kipindi cha miezi michache ijayo, mteja ataweza kujua deni lake na kurejesha kupitia simu ya mkononi.

Pili, kuhusu kutoa mikopo kwa wanafunzi wengi zaidi. Kwa mwaka 2020/2021, wanufaika watakuwa 145,000 wakati mwaka 2014/2015 walikuwa 98,300. Ukusanyaji wa mikopo iliyoiva nao umeongezeka kutoka wastani wa TZS 2 bilioni kwa mwezi mwaka 2015/2016 hadi TZS 17 bilioni kwa mwezi mwaka 2019/2020.

Tatu, mahusiano na wadau wetu yameimarishwa. Wadau hao ni wanafunzi, serikali za wanafunzi na mashirikisho yao – TAHLISO na ZAHLIFE. Wadau wengine ni Waheshimiwa Wabunge, Waajiri, taasisi za fedha na mashirika na taasisi mbalimbali.

Wewe ni mdau muhimu. Tunahitaji maoni yako.

**Katika  
kipindi cha  
miezi michache  
ijayo, mteja ataweza  
kujua deni lake na  
kurejesha kupitia  
simu ya  
mkononi**

**2020/2021,  
wanufaika  
watakuwa  
145,000 wakati  
mwaka 2014/2015  
walikuwa  
98,300.**

**Wadau hao ni  
wanafunzi, serikali  
za wanafunzi na  
mashirikisho yao  
- TAHLISO na  
ZAHLIFE.**

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**  
Omega Ngole

**Wajumbe**  
Veneranda Malima  
Ismail Ngayonga  
Eline Maronga  
Jonathan Nkwabi  
Jacqueline Msuya

**Designer**  
+255 719 190 083

**Mawasiliano**  
Mkurugenzi Mtendaji  
Bodi ya Mikopo ya  
Wanafunzi wa Elimu ya Juu  
1 Mtaa wa Kilimo, TAZARA  
S.L.P 76068  
Dar es salaam  
Tanzania

**WhatsApp:** 0736 665 533  
**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz  
**Tovuti:** heslb.go.tz

**HESLB**

**BODI YA MIKOPO**  
INVESTING IN THE FUTURE







## NIBOYE: Shukrani serikali kwa malipo kwa wakati

*Na Jaqueline Msuya*

**Mwenyekiti** wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Nchini (TAHLISO), Peter Niboye ameishukuru Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kuendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wakati katika vyuo vyote nchini.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa TAHLISO uliofanyika tarehe 19 Desemba mwaka jana Jijini Dar es Salaam, Niboye alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita fedha za mikopo ya elimu ya juu zimekuwa zikilipwa kwa wakati kutokana na Serikali kutambua mchango wa elimu ya juu katika maendeleo ya nchi.

"Vyuo na wanafunzi wamekuwa wakilipwa stahili zao kwa wakati, TAHLISO itaendelea kushirikiana na Serikali za Wanafunzi katika vyuo vyote nchini kuhakikisha kuwa

hali ya utulivu inazidi kuimarika vyaoni na kuendelea kuratibu maoni na malalamiko yao kwa njia ya hekima na busara," alisema Niboye.

Kwa upande wake Mkuu wa Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole alisema dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha wanafunzi wote wenye sifa na ambao wamewasilisha maombi kwa usahihi, wanapata mikopo ya elimu ya juu na hilo linajidhihirisha na ongezeko la bajeti ya mikopo kutoka TZS 348.7 bilioni mwaka 2014/2015 hadi TZS 464 bilioni kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

Ngole aliongeza kuwa TAHLISO ni wadau muhimu wa HESLB na kutokana na umuhimu huo, HESLB imekuwa ikishiriki mikutano ya shirikisho hilo kwa ajili ya kusikiliza changamoto na hoja mbalimbali na kuzitolea majibu na ufafanuzi pale inapohitajika.

**mikopo  
kutoka TZS 348.7b  
mwaka 2014/2015  
hadi TZS 464bn  
kwa mwaka  
wa masomo  
2020/2021**

**Katika  
kipindi cha  
miaka mitano  
iliyopita fedha za  
mikopo ya elimu  
ya juu zimekuwa  
zikilipwa kwa  
wakati**







1



2



3

1. Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (aliyesimama) akimtambulisha Mwenyekiti wa Bodi HESLB, Prof. William Anangisye kwa wajumbe wapya wa bodi hiyo walioteuliwa na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia 2. Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Omary Kipanga akisalimiana na Mkurugenzi wa Uchambuzi na Upangaji Mikopo HESLB, Dkt. Veronica Nyahende wakati wa ziara yake aliyoifanya katika ofisi za HESLB tarehe 4 Januari, mwaka huu. 3. Watumishi wa HESLB wakisikiliza kwa umakini mabimbali zilizokuwa zikiwasilishwa wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyoifanya tarehe 30-31 Januari mwaka huu. 4. Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru akitoa mada kuhusu majukumu ya taasisi hiyo kwa wajumbe wa kamati ya kudumu ya bunge ya huduma za maendeleo ya jamii katika ofisi za ukumbi wa bunge Jijini Dodoma hivi karibuni



4





## KIPANGA: Shirikisheni NIDA, TRA kusaka wadau wa mikopo

*Na Veneranda Malima*

**Naibu** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga ameitaka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kushirikiana na wadau wengine kama Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwasaka wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu wanaodaiwa mikopo ya elimu ya juu.

Akizungumza katika ziara yake ya kwanza ya kikazi aliyoifanya HESLB tarehe 4 Januari, mwaka huu, Naibu Waziri Kipanga alisema HESLB haina budi kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha wadau wa mikopo ya elimu ya juu ambao wengi wao kwa sasa ni waajiriwa katika sekta binafsi wanarejesha mikopo hiyo ili iweze kuwanufaisha wanafunzi wengine.

"Tangu mwaka 1994/1995, Serikali imetumia kiasi cha TZS 4.8 Trilioni kwa ajili ya kugharamia mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi 583,600 na kati ya fedha hizo ni TZS 871.3 Bilioni ndizo zilizorejeshwa hadi sasa kati ya TZS 1.2 trilioni, hivyo hatuna budi kuhakikisha kuwa fedha zilizobaki zinapatikana kutoka kwa wadau sugu" alisema Kipanga.

Naibu Waziri Kipanga alisema NIDA na TRA ni mamlaka za serikali zenye taarifa muhimu na hivyo zinatoa urahisi wa kuwatambua wanufaika wa mikopo iwapo kutakuwa na ushirikiano wa kimkakati.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru alisema tayari mazungumzo ya awali yamefanyika na taasisi hizo kwa lengo la kubadilishana taarifa.

"Tumeanza mazungumzo na wenzetu hao na tunaamini muda si mrefu tutakua na makubaliano rasmi ambayo yataongeza ufanisi kwa kiasi kikubwa," alisema Badru katika kikao cha Naibu Waziri na menejimenti ya HESLB.



**Tangu  
1994/1995  
serikali imetumia  
TZS 4.8tr kwa ajili  
ya kugharamia  
wanafunzi  
583,600**

**Kati ya  
fedha hizo ni  
TZS 871.3bn ndizo  
zilizorejeshwa hadi  
sasa kati ya  
TZS 1.2tr**





# MUSTAFA:

## Nilitimiza wajibu, HESLB ikanipangia mkopo

*Na Ismail Ngayonga*

**Mwanafunzi** Mustafa Emmanuel (22) wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM) amewataka wanafunzi wahitaji wa mikopo ya elimu ya juu nchini kutimiza wajibu wao kwa kuambatisha taarifa sahihi za uhitaji wakati wa dirisha la maombi.

Mwalimu Mustafa Emmanuel, ambaye ni Mtoto wa kwanza wa Bw. Jackson Emmanuel (39) na Zamira Hassan (34), alnasema katika elimu yake ya sekondari ya kidato cha HIV alifadhiliwa na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Tanzania (TASAF) kati ya mwaka 2012 hadi 2016.

Mustafa alishukuru HESLB kufuatia mafunzo ya uombaji mikopo yaliyotolewa na HESLB mwaka 2019, Mkoani Lindi ambapo alishiriki Semina hiyo na kupata uelewa kuhusu mahitaji na nyaraka muhimu zinazohitajika katika uombaji mikopo ikiwemo taarifa za hali ya uhitaji wa mkopo.

"Nilipokuwa Kijijini Kiwalala, nilisikia matangazo ya HESLB kupitia redio, nilihudhuria mafunzo, nilisoma mwongozo, kujaza fomu kwa usahihi na kutuma maombi yangu kwa wakati, nashukuru nikapangiwa mkopo na HESLB" alisema Mwalimu Mustafa.

Mustafa anasema katika majibu ya upangaji mikopo, mwanzoni mwa mwezi Desemba 2019, HESLB ilimpangia mkopo kwa asilimia 100 ikijumuisha ada ya masomo, fedha za chakula na malazi, utafiti, mafunzo kwa vitendo.

Akifafanua zaidi Mustafa anasema mafunzo hayo ni vyema yakawa endelevu kwa wanafunzi waombaji, kwa kuwa yatasaidia kupunguza makosa madogo ikiwemo kutosaini fomu, kutoambatisha nyaraka muhimu n.k.

"Naishukuru HESLB kwa kuniwezesha kufika Chuo Kikuu, napongeza mfumo wa HESLB wa uchambuzi wa uhitaji ikiwemo kutumia TASAF, hili limetusaidia sisi wanafunzi tunaotoka katika familia za kaya maskini kupangiwa mikopo," alisema Mustafa.

alifadhiliwa  
na Mpango wa  
Kunusuru Kaya  
Maskini Tanzania  
(TASAF) kati ya  
mwaka 2012  
hadi 2016

mafunzo  
haya ni vyema  
yakawa endelevu  
kwa wanafunzi  
waombaji, kwa  
kuwa yatasaidia  
kupunguza  
makosa





## ...Waajiri tuoeni kipaumbele makato elimu ya juu

### Inatoka UK1

Aidha aliongeza kuwa Serikali itaendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa HESLB inakuwa na Mfuko endelevu wenye manufaa katika ujenzi wa taifa.

"Nilihakikishie Bunge lako tukufu kwamba Serikali ipo tayari kuendelea kujifunza kutoka kwa wabunge na wananchi wote kuhusu namna bora zaidi ya kuufanya mfuko huu uwe endelevu na wenye manufaa katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu pia aliagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kushirikiana na HESLB kuweka mazingira wezeshi ya urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika walioajiriwa na waliopo sekta binafsi kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu haki na wajibu wa mnufaika na mwajiri.

Majaliwa aliwasihia wanufaika wote, hususani ambao hawajaitokeza kuanza kurejesha mikopo hiyo ambayo ilianza kutolewa na Serikali miaka 15 iliyopita.



## Wanawake HESLB wapongeza uwakilishi kuongezeka

### Na Mwandishi Wetu

**Mwenyekiti** wa Kamati ya Wanawake HESLB, Veneranda Malima ameipongeza menejimenti ya HESLB kwa kutoa kipaumbele cha wanawake katika nafasi za uongozi ndani ya taasisi hiyo.

Akitoa salamu za shukrani kwa mgeni rasmi wakati wa maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani yaliyofanyika Machi 8, 2021 jijini Dar es Salaam, Malima alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita HESLB imepata mafanikio makubwa ya kiutendaji kutokana na mchango uliooneshwa na wanawake.

"Mwaka 2016, uliagiza nafasi za juu za uongozi angalau ziwe na uwakilishi wa wanawake, tunashukuru kwa sasa tuna zaidi ya viongozi 10 wanawake katika menejimenti ya taasisi, hii imetokana na utendaji kazi, ubunifu na maarifa katika sehemu zao za kazi" alisema Veneranda.

Aidha Veneranda aliwaasa watumishi wanawake wa HESLB kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuimarisha mshikamano katika sehemu zao za kazi kwani kwa kufanya hivyo wataweza kufikia malengo mbalimbali yaliyowekwa na taasisi kupitia mpango mkakati wa miaka mitano (2017-2022).

Kauli mbiu ya siku ya wanawake duniani ni "Wanawake katika Uongozi chachu kufikia dunia yenye usawa"



## MTAFYA: DARUSO tupo bega kwa bega na HESLB

### Na Eline Maronga

**Rais** wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DARUSO) Noel Mtafya amewataka wanafunzi wa vyuo vikuu nchini kusoma kwa bidii kwa kuwa Serikali kupitia HESLB imekuwa ikitoa mikopo ya elimu ya juu inayozingatia mahitaji ya makundi yote ya kijamii.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB YAKO, Mtafya anasema kwa sasa fedha za wanafunzi zimekuwa zinawafikia wanafunzi kwa wakati ukilinganisha na kipindi cha miaka ya nyuma ambapo jambo hili lilipelekea kuwa na migomo mingi vyaoni.

"Serikali imeongeza mara dufu bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini kutoka TZS 348.5 Bilioni mwaka 2014/2015 hadi kufikia TZS 464 Bilioni mwaka 2020/2021 ili kukizi mahitaji ya wanafunzi wote, hasa wanaotokea katika familia masikini" alisema Mtafya.

Aidha Mtafya alipongeza maboresho ya mfumo ikiwemo kunzishwa kwa mfumo kwa kusaini fedha kwa alama ya vidole (finger print) umeongeza ufanisi katika kurahisha upatikanaji wa fedha kwa wanafunzi kwa muda mchache sana ukilinganisha na mfumo wa zamani.

Kwa mujibu wa taarifa ya HESLB katika mwaka wa masomo 2020/2021, Serikali imepanga mikopo kwa wanafunzi 15972 wa UDSM wakiwemo wanafunzi 6087 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 9885 wanaoendelea na masomo yenye thamani ya TZS 53.3 Bilioni. Kati ya wanafunzi hao wanawake ni 7291 na wanaume ni 8681.

Serikali katika mwaka wa masomo 2020/2021 ilitenga bajeti ya kiasi cha TZS 464 Bilioni kwa ajili ya kusomesha wanafunzi 145,000 wakiwemo wanafunzi 54000 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 91,000 wanaoendelea na masomo.

Mtafya alipongeza maboresho ya mfumo ikiwemo kunzishwa kwa mfumo kwa kusaini fedha kwa alama ya vidole

Kwa mwaka wa masomo 2020/2021 Serikali imepanga mikopo kwa wanafunzi 15972 wa UDSM

Wanafunzi 6087 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 9885 wanaoendelea na masomo







## VIATORY: Changamoto za kusoma nje ya nchi

*Na Veneranda Malima*

**Serikali** imeombwa kuendelea kupeleka wanafunzi kusoma katika nchi marafiki ili kuongeza upeo na kujiamini kwa wanafunzi wa kitanzania wanaopata nafasi za masomo nje ya nchi.

Akizungumza na HESLB Yako, Rais wa zamani wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania wanaosoma nchini Msumbiji (TASAM), Viatory Kazana Mnyaga amesema kuwa kwake fursa hiyo ya masomo nchini Msumbiji katika Chuo Kikuu cha Pedagogica kilichopo Maputo, imemuwezesha kujifunza na kuongea lugha ya Kireno, kukutana na watu wa mataifa mbalimbali duniani na kuongeza kujiamini na stadi za uongozi.

Aidha Mnyaga amepongeza utaratibu wa utoaji wa mikopo nchini Tanzania akilinganisha na Msumbiji ingawa nchi zote mbili zinawalenga wanafunzi wahitaji; amesema Tanzania imesonga mbele zaidi kwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaonufaika na jinsi mikopo hiyo inavyosimamiwa ili kuwafikia walengwa.

Mnyaga amesoma shahada ya Uongozi wa Elimu (2013-2019) na Serikali ya Tanzania kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imemlipia gharama zote za nauli ya kwenda na kurudi, ada ya mafunzo na fedha za kujikimu kwa kipindi cha miaka mitano; ukiwemo mmoja wa kujifunza lugha.

Serikali za Tanzania na Msumbiji zimekuwa na Mpango wa kubadilishana wanafunzi wa vyuo vikuu (Tanzania - Mozambique Students Exchange Programme - TAMOSE) unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.



## Wajibu wa mnufaika wa mkopo

1. Hakikisha unamuona Afisa Mikopo wa Chuo chako kufahamu utaratibu wa kupokea fedha za mkopo;
2. Iwapo mkopo wako upo katika chuo kingine, hakikisha unawasiliana na Afisa Mikopo wa chuo chako ili kukamilisha taratibu wa uhamisho wa mkopo wako;
3. Fungua akaunti kwenye benki uipendayo na wasilisha taarifa za akaunti hiyo kwa Afisa Mikopo;
4. Hakikisha umesaini nyaraka muhimu kwa Afisa Mikopo ili kuthibitisha kupokea fedha;
5. Ikiwa hujajisajili na mfumo wa malipo wa DiDiS (Digital Disbursement Solution), ni muhimu sana kujisajili ili unufaike na faida zake ikiwemo kupokea fedha kwa haraka;
6. Fedha utakazopokea ni mkopo, tumia kama ilivyokusudiwa



## Wajibu wa mwajiri

1. Hakikisha unawasilisha majina ya wafanyakazi wako wapya kwa HESLB katika kipindi cha siku 28 tangu waajiriwe;
2. HESLB itachambua orodha na kukujulisha iwapo kuna wanufaika na utaratibu wa kuwasilisha makato yao ndani ya siku 15 baada ya mwisho wa mwezi;
3. Marejesho yote yatafanywa kwa njia ya GePG kwa kutumia Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (Control Number);
4. Tembelea [www.heslb.go.tz](http://www.heslb.go.tz) na fungua 'Waajiri' au 'Employers' ili kupata utaratibu wa kurejesha.





## Urejeshaji mikopo kwa 'diaspora' warahisishwa

*Na Jaqueline Msuya*

**Bodi** ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ipo mbioni kuzindua mfumo mpya wa urejeshaji mikopo kwa njia ya mtandao kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu waliopo nje ya nchi (ughaibuni).

Mkurugenzi wa Urejeshaji Mikopo wa HESLB, George Mziray ameiambia 'HESLB Yako' kuwa mfumo huo mpya utaanza kufanya kazi mwezi Machi mwaka huu ambapo mnufaika au mwajiri atapaswa kuingia katika tovuti ya HESLB ([www.heslb.go.tz](http://www.heslb.go.tz)) na kufuata maelekezo rahisi ya utaratibu wa kurejesha kutoka popote alipo, ndani au nje ya nchi.

Mziray amesema kupitia mfumo huo, mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu aliyopo nje ya nchi ataweza kurejesha mkopo baada ya kujisajili kwa kutumia namba ya kidato cha nne na kupata namba ya malipo (Control Number).

"Ikiwa amesahau namba ya mtihani wa kidato cha nne, ataweza kuitafuta cha kutumia majina yake na chuo alichosoma ... na kufuata maelekezo rahisi ya namna ya kurejesha kutoka nchi yoyote alipo," amesema Mziray.

Mziray amesema hatua ya kuanzishwa kwa mfumo huo imetokana na maoni ya wanufaika wengi waliopo nje ya nchi ambao walishauri kurahisishwa kwa njia za malipo.

"Mfumo huu pia utawawezesha waajiri waliopo nchini kuingia katika tovuti na kujisajili kwa kutumia TIN (Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi) na kuwasilisha makato ya wanufaika ambao ni wafanyakazi wao," amesema.

CRDB Bank Acc.  
Na. 01j1028467503

SWIFT CODE:  
CORUTZT

NMB Bank Acc.  
Na. 20101100205

SWIFT CODE:  
NMIBTZZ


TPB Bank Acc.  
Na. 110208000002

SWIFT CODE:  
TAPBTZZ





## DiDiS ndio mpango mzima



*Na Jacqueline Msuya*

**Ni** mfumo mpya wa malipo ya fedha za mikopo kwa wanafunzi kwa kutumia biometriki na kumuwezesha mnufaika kupokea fedha ndani ya dakika tano tangu kusaini kwa vidole.

Mfumo huu ambao kwa kiingereza unafahamika kama 'Digital Disbursement Solution' ulianza kwa majaribio katika vyuo vichache mwaka 2017/2018 na baada ya mafanikio, ukaendelezwa katika vyuo vyote nchini.

"Hadi kufikia Februari 2021, wanafunzi wanufaika 65,638 ambao ni asilimia 45 ya wanufaika wote waliopo vyaoni wanapokea fedha kwa kutumia mfumo huu," anasema Sara Fihavango, Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia malipo ya wanafunzi.

"Tunaendelea kusajili waliobaki na baada ya kukamilisha, malipo yote yatafanywa kupitia mfumo huu ndiyo sababu tunawakumbusha wateja wetu kuhakikisha wanajisajili katika mfumo huu," anaongeza Sara.

Kwa mujibu wa Sara, ili kujisajili katika mfumo huu, mwanafunzi anapaswa kuwa na akaunti katika benki aipendayo na kupokea maelezo kupitia ofisa mikopo wa chuo chake ambaye ameelelimesha kuhusu mfumo huu.

"DiDiS ndiyo mpango mzima na ndiyo sababu tumejipanga kuachana kabisa na mfumo wa malipo kwa njia ya makaratasi, hivyo zoezi hili la usajili ni la lazima na itakuwa vigumu kwa mwanafunzi asiyejisajili kuweza kulipwa fedha za mkopo katika awamu zijazo" anasema Sara.

# DiDiS

Digital Disbursement Solution

Mfumo wa  
**DiDiS** ulianza  
kutumika kwa  
majaribio katika  
mwaka wa masomo  
**2017/2018** katika  
vyuo **24**





## HESLB: Tutaendeleza mashirikiano na wadau



*Na Ismail Ngayonga*

**Bodi** ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema itaendelea kuimarisha mahusiano ya kimkakati na wadau wake ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu majukumu ya taasisi hiyo.

Akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Nchini (TAHOSSA) uliofanyika tarehe 20-22 Desemba, 2020 Jijini Dodoma, Mkuu wa Mawasiliano wa HESLB, Omega Ngole alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita HESLB imepata mafanikio makubwa kutokana na mashirikiano na wadau.

Akitolea mfano, Ngole anasema HESLB, imeendelea kuongeza kiwango cha makusanyo ya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika mwaka hadi mwaka kutoka TZS 28/- Bilioni mwaka 2015/2016 hadi TZS Bilioni 192.10/- mwaka 2019/2020, juhudi zilizotokana na mashirikiano na wadau mbalimbali.

"TAHOSSA ni wadau muhimu sana kwetu, tunaposema tumeongeza makusanyo ya mikopo iliyoiva kutoka wastani wa TZS 2 Bilioni kwa mwezi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita hadi wastani wa TZS 17 Bilioni kwa mwezi, haya ni mafanikio yaliyotokana na ushirikiano na wadau wetu ikiwemo TAHOSSA" alisema Ngole.

Aidha Ngole anasema HESLB imetumia fursa ya mkutano huo kwa ajili ya kutoa ufafanuzi na kujibu hoja mbalimbali zinazotolewa na watumishi mbalimbali wa sekta za umma na binafsi wakiwemo walimu kuhusiana na tozo ya makato ya mishahara kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na HESLB.

"Kwa sasa tunakusanya asilimia 42 ya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika, tumejiwekea malengo kupitia Mpango mkakati wa taasisi hadi kufikia mwaka 2023 tuwe tunakusanya asilimia 60 ya mikopo iliyoiva na kuweka mkakati wa kufikia kiwango cha asilimia 50 cha urejeshaji wa mikopo kwa hiari kutoka kwa wanufaika" alisema Ngole.

Tumeongeza makusanyo kutoka TZS 28bn mwaka 2015/2016 hadi TZS 192.10bn mwaka 2019/2020

haya ni mafanikio yaliyotokana na ushirikiano na wadau wetu ikiwemo TAHOSSA"

Mpango mkakati wa taasisi hadi kufikia mwaka 2023 tuwe tunakusanya asilimia 60 ya mikopo iliyoiva



Tozo  
ya Kutunza  
Thamani ya  
Fedha 6%  
katika salio  
la deni

Adhabu  
ya 10% kwa  
mnufaika  
baada ya  
miezi 24

Tozo ya  
Uendeshaji 1%  
ya deni la  
msingi kwa  
shughuli za  
uendeshaji

## TOZO ZA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

**Mikopo** ya wanafunzi wa elimu ya Juu ina tozo wakati wa kurejesha baada ya mnufaika kuhitimu au kukatisha masomo yake zinazowahusu wanufaika na wajiri wao ili kuufanya Mfuko wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kuwa endelevu.

Tozo hizo ni pamoja na:

1. Tozo ya kutunza Thamani ya Fedha (Value Retention Fee) hutozwa 6% katika salio la deni (Outstanding Loan Balance) kwa mwaka. Ilianzishwa ili kutunza thamani ya fedha za mikopo zinazotolewa kwa wanufaika.
2. Adhabu (Penalty) hutozwa 10% kwenye deni la mnufaika aliyechelewa kuanza kurejesha mikopo wake ndani ya miezi 24 baada ya kuhitimu masomo yake.
3. Tozo ya Uendeshaji (Loan Administration Fee) hutozwa 1% ya deni la msingi (Principal Loan) la mnufaika ili kuwezesha shughuli za uendeshaji zikiwemo kuboresha mifumo ya TEHAMA na kutafuta wanufaika.

Mabadiliko ya Sheria ya 2016, yanatamka makato ya 15% kwa mnufaika aliyejajiriwa na shilingi 100,000/= au 10% ya mapato kutoka kwa mnufaika aliyejajiriwa na yameongeza muda wa matazamio kutoka miezi 12 hadi miezi 24.

## OFISI ZETU

### DAR ES SALAAM

BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI ELIMU YA JUU  
HESLB HOUSE, 1 MTAU WA KILIMO, TAZARA, BR. MANDELA.  
S.L.P 76068, 15471 DAR ES SALAAM  
0736 665533 | 0739 665533  
INFO@HESLB.GO.TZ

### DODOMA

JENGO LA CAG, GHOROFYA YA CHINI,  
S.L.P 984, DODOMA,  
SIMU: 0758 067 577 | 0739 067 577  
DODOMA@HESLB.GO.TZ

### ZANZIBAR

JENGO LA ZSTC, KINAZINI, BR. MALAWI,  
S.L.P 900, ZANZIBAR,  
SIMU: 0779 321 424  
ZANZIBAR@HESLB.GO.TZ

### ARUSHA

NSSF JENGO LA MAFAO, GHOROFYA YA KWANZA,  
S.L.P 2712, ARUSHA,  
SIMU: 027 2520128 | 0624 100011 | 0739 102016  
ARUSHA@HESLB.GO.TZ

### MWANZA

PSSSF PLAZA, GHOROFYA YA PILI,  
FRONT WING, BR. KENYATTA, S.L.P 3051, MWANZA,  
SIMU: 028 2506008 | 0759 819350 | 0738 153661  
MWANZA@HESLB.GO.TZ

### MBEYA

JENGO LA CAG, BR. MBALIZI,  
S.L.P 319, MBEYA,  
SIMU: 0738 131310 | 0738 131311  
MBEYA@HESLB.GO.TZ

### MTWARA

NHC RAHA LEO COMPLEX GHOROFYA YA PILI  
KIWANJA NA. 217 KITALU H,  
KARIBU NA OFISI YA MKUU WA MKOA  
S.L.P 969, MTWARA, SIMU: 0736 026 668  
MTWARA@HESLB.GO.TZ